HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA
UPIMAJI WA WILAYA WA KIDATO CHA PILI
SEPTEMBA 2026

021 **KISWAHILI**

MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

SEHEMU A: MAARIFA NA UFAHAMU

1.

I	II	III	IV	V	VI	VII	VIII	IX	X
B	**A**	**B**	**B**	**A**	**C**	**B**	**B**	**B**	**C**

2. Majibu ya Kuoanisha

I	II	III	IV	V
C	**G**	**B**	**D**	**F**

SEHEMU B: UPIMAJI WA UMAHIRI

3. (a) Maana ya Utamaduni: Ni mfumo mzima wa maisha ya jamii ya Kitanzania ikijumuisha lugha, mila, desturi, amali, sanaa, mavazi, imani na namna wanavyotatua changamoto zao mbalimbali za kila siku.

(b) Mambo yanayounda utamaduni (Taja manne miongoni mwa haya):

i. Lugha (k.m. Kiswahili)
ii. Mavazi ya kitaifa au ya kiasili
iii. Mila na desturi (k.m. salamu, jinsi ya kulea watoto)
iv. Sanaa (k.m. muziki wa asili, michoro, kazi za mikono)
v. Chakula cha asili
vi. Imani na maadili ya jamii

4. i. Mti **huu umekatwa** jana.
ii. Watoto **wote** wamecheza vizuri.
iii. Nyumba **ambayo** ilijengwa imeanguka.
iv. Kalamu zangu mbili **zimepotea**.
v. Chakula kile kilikuwa **kitamu** sana.

Shulelibrary.com

5. **(a) Maana ya Neno Kiongozi:** Ni neno linalochapishwa juu kabisa ya ukurasa wa kamusi (kushoto au kulia) ili kumwonyesha mtumiaji neno la kwanza au la mwisho linalopatikana katika ukurasa huo, hivyo kumsaidia kupata neno analolitafuta kwa haraka.

- **(b) Kazi nyingine za kamusi (Taja nne miongoni mwa hizi):**
  i. Kuonyesha tahajia (uandishi sahihi wa maneno)
  ii. Kuonyesha aina za maneno au sarufi (k.m. nomino, kitenzi, kivumishi)
  iii. Kuonyesha namna neno linavyotamkwa
  iv. Kuonyesha asili au chimbuko la neno
  v. Kuonyesha kisawe au kinyume cha neon

6. **Uanganuaji wa Mofimu za Neno "Walivyocheza"**
   (Mchanganuo: Wa-li-vyo-chez-a)
   (i) Kiambishi awali cha nafsi/ngeli: **Wa-**
   (ii) Kiambishi cha wakati: **-li-**
   (iii) Kiambishi cha kurejea: **-vyo-**
   (iv) Mzizi wa neno: **-chez-**
   (v) Kiambishi tamati: **-a**

7. **Kuunda Sentensi Changamani**
(i) Mwanafunzi **anayesoma** kwa bidii atafaulu. *(au: Mwanafunzi atafaulu **ikiwa** anasoma kwa bidii.)*
(ii) Juma alichelewa shuleni **kwa sababu** gari liliharibika njiani. *(au: Gari liliharibika njiani **ndiyo maana** Juma alichelewa shuleni.)*

8. **Kanuni za Adabu na Ufasaha (Mambo ya kuzingatia)**
(Taja manne miongoni mwa haya au yanayoshabihiana nayo):
   i. Kutumia salamu ya heshima kulingana na utamaduni (k.m. Shikamoo).
   ii. Kutumia lugha yenye staha, unyenyekevu na adabu (epuka maneno ya dharau au mitaani).
   iii. Kusikiliza kwa makini bila kumkatiza mzungumzaji aliyekuzidi umri.
   iv. Kudhibiti lugha ya mwili (k.m. kutokumkodolea macho kwa ukali au kukunja mikono kifuani kwa ishara ya ukaidi).
   v. Kutumia sauti ya wastani (kutopiga kelele wala kunong'ona kupitiliza).

Shuleilibrary.com

9. Ufahamu

- **(a) Kichwa cha habari kinachofaa:** Lugha ya Kiswahili na Utamaduni Wetu / Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili / Kiswahili na Maadili ya Kitanzania. *(Kichwa chochote chenye mashiko na kifungu kinakubalika).*
- **(b) Kitakachotokea:** Kutatokea mmomonyoko wa maadili katika jamii unaosababishwa na kasumba za kigeni.
- **(c) Kisawe cha neno "Kasumba":** Ulimbukeni, athari ya kiutamaduni, fikra duni za kuiga, au mtazamo hasi wa kuiga mambo ya kigeni.

SEHEMU C: (ALAMA 15)

10. Mwanafunzi anapaswa kuchagua na kujibu swali **MOJA** tu kati ya yafuatayo:

- **(a) Hotuba:**
  - **Muundo:** Izingatie muundo wa hotuba unaojumuisha kichwa cha hotuba, utangulizi/salamu za protokali (kuwataja viongozi na wageni waalikwa kwa vyeo vyao), kiini cha hotuba (kufafanua umuhimu wa Kiswahili katika kuleta umoja wa kitaifa kama vile kuondoa ukabila, kurahisisha mawasiliano na kujenga utambulisho mmoja), na hitimisho (shukrani).
  - **Maudhui na Lugha:** Hoja zijieleze vizuri, lugha iwe ya kuvutia na inayolenga hadhira ya mahafali.

- **(b) Barua ya Kirafiki:**
  - **Muundo:** Izingatie muundo wa barua zisizo rasmi: Anwani ya mwandishi (juu upande wa kulia), tarehe, salamu ya kirafiki (k.m. Mpendwa..., Kwa rafiki yangu...), sehemu ya kiini/ujumbe, na hitimisho la kirafiki pamoja na jina la mwandishi (chini upande wa kulia).
  - **Maudhui:** Barua ieleze maandalizi ya masomo ya Kidato cha Pili (k.m. kujisomea kwa vikundi, kufanya maswali ya mitihani iliyopita) na malengo ya mtihani wa Taifa wa FTNA (k.m. kufaulu kwa kiwango cha juu/Daraja la Kwanza).

shulelibrary.com